# Learning by Ear 2012 – Corruption – The Elephant in the Room

## Episode 01 – "At School, At Work and Everywhere"

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**Translating: Eric Ponda**

CHARACTERS:

Intro:

- NARRATOR

Scene 1:

- LYDIA (FEMALE, 16 YEARS)
- JENNIFER (FEMALE, 55 YEARS)
- NARRATOR

Scene 2:

- MR MWICHULI (MALE, 50 YEARS)
- ALFAYO (MALE, 58 YEARS)

Outro:

NARRATOR

**Intro:**

**0. Narrator:**

Hujambo na kwa mara nyingine tena karibu kwenye awamu nyingine ya mfululizo wa vipindi vya ‘Learning By Ear’ “Noa Bongo Jenga Maisha yako”. Huu ni mchezo wa redio unaozungumzia suala la Ulaji rushwa ambalo limekuwa kikwazo kwa jamii. Katika vipindi kumi vilivyoko kwenye mchezo huu kwa jina “Tembo Nyumbani” tutaangazia ni kwa jinsi gani ufisadi ulivyokita mizizi barani Africa na kuathiri maisha ya mwanadamu, japo ni tatizo linaloweza kuepukw au kuangamizwa.
Familia ya Odhiambo ni mfano mzuri miongoni mwa familia nyingi za Africa, inayohitaji pesa za matumizi, kusomesha watoto na kuishi maisha ya kadri, licha ya kwamba inaishi katika mazingira yaliyojaa ufisadi. Wanajaribu kuishi maisha ya kawaida pasi na kujihusisha na ufisadi,lakini kwa hakika ni mtihani mkubwa kwao.
Na kama mtakavyo sikia katika vipindi vitakavyofuata, Familia hii inakabiliwa na changamoto nyingi na vishawishi vya kutoa au kupokea rushwa kama njia ya mkato maishani. Hata hivyo inapinga vikali njia hizi za mkato na kudumisha msimamo mkali licha ya kwamba wanaojaribu kuwahonga ni wafanyi biashara na wanasiasa mashuhuri wenye ushawishi mkubwa.

Katika kipindi hiki cha kwanza kwa Jina, “Kazini, Shuleni na kila Mahali”, Lydia,kitinda mimba katika familia ya Odhiambo,ya watoto watatu, anafahamu kwamba ufisadi umekithiri shuleni mwao.

**<u>Scene One:</u>**

**1. SFX:** **Radio on in the house. Noises of someone cooking. Door opens and slams shut.**

**2. LYDIA:** Mama! Mama, uko wapi?Uko ndani?

**3. JENNIFER:** Ndio.. niko hapa jikoni. Lydia, kuna nini?

**4. LYDIA:** Nimeghadhabika! Nimekasirika sana mama!

**5. JENNIFER:** Kwanini Lydia,kumetokea nini?  Au hukufanya vizuri shuleni?

**6. LYDIA:** Oh, Ni zaidi ya hayo Mama! Ehhh .. ni kweli sikufanya vizuri kama nilivyotarajia katika mtihani wangu wa mwishoni mwa mwaka, lakini naamini nilipasa kupata alama za nzuri zaidi kuliko zile nilizopewa na Mwalimu. Lakini cha kusikitisha na kinachoniudhi zaidi ni kwamba baadhi ya wanafunzi wavivu na wajinga kabisa darasani mwetu ndio waliopata alama za juu zaidi. Wanafunzi ambao hawajishughuliki na chochote katika masomo yao!

**7. JENNIFER:** Sasa ni vipi waliweza kupata alama za juu zaidi?

**KW begin**

**8. LYDIA:** Rushwa!

**9. JENNIFER:** Rushwa? Unamaanisha nini?

**KW end**

**10. LYDIA:** Yote hayo huanzia kwa wazazi – ni jambo la kawaida hasa miongoni mwa watu matajiri - huwapendi kuwaona watoto wao wakifanya vibaya shuleni hata kama ni wajinga na wazembe vipi.Hivyo wazazi watafanya kila hila ikiwa ni pamoja na kuhonga Waalimu ili wapate alama nzuri.

**11. JENNIFER:** Lakini huo ni ufisadi!

**12. LYDIA:** Ndio maanake Mama!. Na kasumba hii imekuwa ikiendelea kwa miaka mingi shuleni.Nilikuwa nikizungumza na Tekla, hakuamini nilipomweleza kwamba sijawahi kushuhudia uovu huu! Sijawahi kufikiria kwamba Waalimu wanaweza kuchukua hongo! Yaani wewe ni mwalimu na unakula rushwa? Nasikia tabia hii imekita mizizi sana? Na hata labda uovu huu unafanyika peupe shuleni mwako Mama.

**13. JENNIFER:** Lydia Kwa hakika Lydia, kama kuna ufisadi shuleni mwangu siwezi kujua.Sijawahi kulizungumzia suala hili na waalimu yoyote shuleni. Pengine hata limenitokea na sina habari wala nia ya kulifuatilia.Sijawahi kumuuliza Mtu yoyote kuhusu suala hili.

**14. LYDIA:** Kwa hiyo huenda kuna ufisadi shuleni mwaka?

**15. JENNIFER:** Pengine, sina hakika.

**16. LYDIA:** Lakini hii ni tabia mbaya sana!

**KW begin**

Endapo kuna wanafunzi wanaotoa hongo ili kupata alama nzuri wanazohitaji, ni kumaanisha matokeo ya mtihani huwa hayana maana yoyote, wala juhudi Mtu masomoni. Bali itategemea tu uzito wa mfuko wa Mtu.Ni tabia mbaya sana. Nilidhani ni wanasiasa pekee wanaojihusisha na ufisadi kwa kila tiku wanachofanya, hata misaada ya kigeni inayopitia mikononi mwao. Lakini kumbe umo shuleni.

**KW end**

**17. JENNIFER:** Yasikitisha sana Lydia, kwa wengi, haya ndio maisha!. Lakini sisemi kwamba tuwaige!. Nakumbuka Babangu alikuwa akisema, ufisadi ni kama "Tembo Chumbani". Hakuna mtu anayetaka kulizungumzia wazi suala hili.Lakini si waona ni tatizo kubwa! Tena kubwa zaidi ya unavyodhania.

**18. LYDIA:** Lakini naamini kunao watu miongoni mwetu ambao wamejitolea kuukemea ufisadi.

**19. JENNIFER:** Ni kweli, wako! Na lazima tuwe na imani kwamba kuna watu wengi wanaozingatia sheria, badala ya kujihusisha katika visa vya ufisadi.

**20. LYDIA:** Lakini Mama, kama hii ndio tabia ya watu, hasa waalimu ambao wanapasa kuwa mfano bora kwa jamii - ni vipi nitaweza kupata alama nzuri zinazohitajika kunipeleka hadi chuo kikuu bila ya kuwahonga waalimu?

**21. JENNIFER:** Usiwe na wasi wasi, wewe ni msichana mwerevu sana Lydia!. Na hakika unafanya bidii katika masomo yako..! na kwasababu hiyo, utafaulu kujiunga na chuo kikuu!.Subiri tu utaona matokeo!. Bidii ndio msingi wa ufanisi wala sivinginevyo. Hilo nakuhakikishia.

**22. LYDIA:** Hmm. Sioni nikifaulu! Oh, suala hili linanitatiza sana.

**End of Scene 1**

**23. NARRATOR:** Kama tulivyosikia, ufisadi umeenea hadi shuleni. Lydia anashtuka kusikia hivyo.Na anaamua kumuuliza mwalimu wake kuhusu suala hili.

Wakati huo huo huo, Alfayo Odhiambo, babake Lydia amegundua ufisadi unaoendelea katika sekta ya kawi. Kampuni ya Alfanyo ndiyo iliyopewa kandarasi ya kuuza vifaa vya mita za umeme katika wizara ya kawi. Katika muda wa miaka michache iliyopita, kampuni yake imepata kandarasi kubwa kubwa na inafanya vyema sana. Lakini kwa mshangao, anagundua kwamba baadhi ya kampuni

anazoziuzia vifaa hivi ni kampuni bandia .Ni majina tu, wala hakuna chochote kinachoendelea.

**Scene 2: Alfayo's Office**

**24. ALFAYO:** **(on the phone)** Kwa hivyo unachomaanisha Bw Mwichuli ni kwamba mita zote nilizowasilisha bado zinalala kwenye ghala? Hazijawekwa kwenye majengo - wala kutumika mahali popote, zipo tu zimelala?

**25. MR MWICHULI:** Nadhani umenisikia vizuri,.. kwani huelewi Bw Alfayo? Hii ni njama tu! Sisi tumefungua kampuni nyingi bandia na kupewa kandarasi kubwa kubwa za mamimilioni ya fedha. Kampuni hizi zinapasa kuwa zinasambaza kiwango fulani cha kawi kote nchini. Na tunahitaji vifaa vyako ili isionekane tunafanya ulagha.

**26. ALFAYO:** Kwa hiyo unasema kuwa kampuni yangu pia iko kwenye mkumbo wa kashfa hii Bw Mwichuli?

**27. MR MWICHULI:** Hasa bila shaka uko katika njama hii. Na ukitaka kampuni yako iendelee kupata faida kubwa, unachohitajika kufanya, ni kuendelea kuweka sahihihi

kandarasi tunazokupa bila ya kuuliza maswali mengi. Hebu fikiria pesa unazopata Bw Alfayo!

**28. ALFAYO:** Lakini mimi singependa kuhusishwa katika kashfa hii.Hii ni biashara niliyorithi kutoka kwa marehemu Babangu. Kwa juhudi zake alifanya kila juhudi kuistawisha na kudumisha jina zuri, na singependa kufanya kinyume na ya hayo kuona jina la kampuni hii likiharibika. Mimi si mfisadi, unanielewa Bw Mwichuli?

**29. MR MWICHULI: (pause)** Kwa hakika sidhani kama msimamo wako unaweza kukusaidia kujitoa katika mambo haya Bw Alfayo. **(pause)** Upende usipende tayari umo kwenye mtego huu. **(getting tough)** Na kuna watu wenye uwezo ambao pia.. wamo katika mpango huu , Alfayo. Na wanaweza kukutia kuweka mashakani. Nakupa muda wa kulifikiria jambo hili. **(pause)** Kisha nitawasiliana nawe baadaye. **(line goes dead)**

**30. SFX:** **Putting down the phone**

**31. ALFAYO:** **(Pacing up and down the room talking to himself)** Sasa nitafanya nini? Siwezi kuendelea kuwauzia bidhaa zangu hasa baada ya kufahamu yote yanayoendelea. Nilianza kushuku mambo haya miezi sita iliyopita, na kisha nikaendelea kukubali kandarasi zao. Sasa hakika mambo yamebadilika. Nitasema nini kwa familia yangu? Najihisi kuwa mdanganyifu? **(pause)** Ghafla biashara yangu ilianza kustawi , kumbe yote yalikuwa ni kutokana na ulaghai huu. Ni sakata ambayo itaweza kuripuka muda si mrefu. Hapana- siwezi kujihusisha na mchezo huu mbaya. Nitazungumza na rafiki yangu Jeffrey aweze kunishauri zaidi.

***KW begins***

**32. SFX:** **Opens door of his office**

**33. ALFAYO:** **(calling to his secretary)** Brenda! Tafadhali unaweza kumpigia simu Jeffrey wa bodi ya kupambana na ufisadi? Mwambie ningependa kuzungumza naye, na tena kwa dharura sana.

***KW ends*** **(to himself)** Hasa! Jeffrey ndiye anayefa kabisa kunishauri kuhusu suala hili. Yeye ataweza kunieleza hatari iliyopo. Mungu wangu balaa gani hii?

**End of Scene 2**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**34. NARRATOR:** Na hadi hapo tunafika tamati ya makala hii ya leo kwenye mchezo wa redio kuhusu Ufisadi kwa jina "Tembo Chumbani'. Hadhithi inayoelezea maisha halisi. Na kama tulivyosikia, Familia ya Odhiambo, haiwezi kupuuza jinamizi hili la ufisadi au "Tembo huyu Chumbani" . Ufisadi unaathiri pakubwa maisha yao sio tu kazini bali hata shuleni pia.Lakini ni vipi watakabiliana na jinamizi hili, Ufisadi?

Katika makala ijayo, tutaskia jinsi bodi ya kupambana na ufisadi itakavyotikiswa, huku Mwana wa kiume wa Odhiambo akikamatwa baada ya kupatikana akiongea na simu anapoendesha gari. Je atawahonga maafisa wa usalama? Ili kupata uhondo zaidi ungana nasi katika

kipindi kinachofuata. Na endapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki, basi tembelea mtandao wetu www.dw.de/lbe. Pia unaweza kututumia maoni yako kupitia Facebook. Hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa!